

## **KAHAWA, KARAFUU, TUMBAKU NA CHIKICHI KUIMARISHA UCHUMI WA MKOA WA MOROGORO**

Mkoa wa Morogoro umejipanga kuimarisha sekta ya kilimo kimkoa kwa kufufua zao la kahawa, kuongeza uzalishaji wa zao la karafuu, kuanzisha kitalu cha miche ya tumbaku, na kuanzisha kilimo cha zao la chikichi.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mheshimiwa Adam Malima wakati alipokuwa akitoa salamu za mkoa kwenye uzinduzi wa maonesho ya NaneNane Kanda ya Mashariki uliofanyika katika uwanja wa J.K Nyerere Morogoro hapo jana tarehe 01.08.2023.



“Miaka ya zamani kahawa aina ya Arabika ilikuwa inalimwa kwenye vijiji vya matombo na kwa upande wa zao la karafuu hata sasa mkoa wetu ndio unashika nafasi ya pili baada ya Zanzibar katika uzalishaji wa zao hilo nchini hivyo ni lazima tuongeze uzalishaji wa zao hilo. Vilevile tunaanzisha kitalu cha tumbaku katika kijiji cha Mvuha ili nasi tuuze tumbaku yetu kwenye kiwanda kikubwa cha tumbaku kilichopo hapa mkoani kwetu kwani kwa sasa zao la tumbaku halilimwi ndani ya mkoa wetu na kama haitoshi, mwanzoni mwa mwezi wa tisa tunatazamia kuzindua ugawaji bure wa miche ya michikichi kwa wananchi ili kuweza kuanzisha kilimo cha zao hilo mkoani mwetu” alifafanua Malima.



Kwa upande mwingine, Mheshimiwa Malima amesema katika kuhakikisha sekta za mifugo na uvuvi nazo zinaimarika, Mkoa wa Morogoro unahamasisha ufugaji biashara na kwa kushirikiana na Wizara ya Uvuvi, Mkoa unapanga kuanzisha uvuvi wa kisasa katika bonde la mto Kilombero ambako samaki aina ya kitoga anapatikana kwa wingi.

Aidha Mheshimiwa Malima amesema, Mkoa unapanga kufanya hayo yote kwa sababu kilimo ndio uti wa mgongo wa Mkoa wa Morogoro na takwimu zinaonesha kwamba Kanda ya Mashariki ndio Kanda kiongozi katika uzalishaji wa miwa, mpunga na mkonge hapa nchini hivyo kwa kuongeza mazao hayo ya karafuu, chikichi, kahawa na tumbaku kutaiongezea sifa Kanda hii na kuimarisha zaidi uchumi wake.

**MWISHO**